



Taarifa kwa vyombo vya habari  
Imezuiliwa hadi tarehe 6 Mei, 2014

## **Huduma na matibabu ya bure inavyowagharimu wazee na watoto**

**Kunyume na Sera, wananchi waripoti kuendelea kutozwa pesa kwa huduma za wagonjwa wa nje.**

**6 Mei 2014, Dar es Salaam:** Ni mtu 1 tu kati ya watu 20 (6%) mwenye umri zaidi ya miaka 60 na ni mtoto 1 kati ya 5 (18%) mwenye umri chini ya miaka mitano ambao hupata huduma na matibabu bure katika vituo vya afya. Sera ya Serikali inasema kuwa huduma kwa wagonjwa wa nje kutoka makundi haya mawili ni bure, lakini wananchi wanasema kuwa wanatozwa pesa.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza katika muhtasari wa utafiti wenye jina la *Je, vituo vya afya vipo kwa ajili ya kuwahudumia watu? Wananchi na watumishi wa afya wazungumzia huduma za afya.* Muhtasari huu ni kwa mujibu wa takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti kwa njia ya simu za mkononi, wenye uwakilishi wa kitaifa uliofanyika kwenye kaya zote Tanzania Bara.

Huduma za afya ni muhimu kwa kuwa zinahitajika sana na wananchi wengi. Zaidi ya nusu (57%) ya Watanzania waliotembelea vituo vya afya kati ya mwezi Mei na Juni 2013 walifanya hivyo kwa dhumuni la kutibiwa wao wenyewe au kumsindikiza mgonjwa. Watu walio wengi (77%) walitembelea zaidi vituo vya afya vya Serikali kuliko vya binafsi au vya dini. Hata hivyo, Watanzania wengi (63%) wanaamini kuwa Serikali inashughulikia vibaya suala la uboreshaji wa huduma za afya. Upatikanaji wa huduma za afya kwa kiasi kikubwa hutegemea uwepo wa watumishi wa afya na upatikanaji wa madawa. Mwezi Septemba 2013, *Sauti za Wananchi* iliripoti kuwa wagonjwa asilimia 41 hawakuweza kupata dawa kwenye vituo vya afya.

Hali siyo tofauti sana linapokuja suala la watumishi wa afya. Zahanati na vituo vya afya vina upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Katika sehemu kubwa ya nchi, vituo vinaendeshwa vikiwa na nusu ya idadi ya watumishi iliyopendekezwa na Serikali kwa watumishi wa kada za waganga na wauguzi. Theluthi moja (31%) ya watumishi hawakuwepo vituoni siku vituo vilipotembelewa na pia ilibainika kuwa hawakutoa taarifa ya kutokuhudhuria kwao. Upungufu wawatumishi walioajiriwa na kutokuwepo kwao kazini vinaweza kusababisha wagonjwa kusubiri kwa muda mrefu na pia kupata huduma duni.

Wagonjwa wengi (70%) wanaotembelea vituo vya afya vya Serikali wanalazimika kusubiri kwa muda wa zaidi ya dakika 30 ndipo wahudumiwe. Hii ni tofauti na vituo binafsi ambapo chini ya nusu (45%) ya wagonjwa husubiri kwa muda huo huo. Aidha, zaidi ya nusu (53%) ya wagonjwa wote wanaotembelea vituo vya afya vyovyote hulazimika kusafiri kwa zaidi ya dakika 30 hadi kukifikia kituo cha afya.

*"Wagonjwa wananyimwa haki zao za kupata huduma kamilifu za kiafya kutokana na uhaba wa madawa muhimu, upungufu wa wafanyakazi na utoro wa watumishi." Alisema Elvis Mushi, Mtafiti kutoka Twaweza. "Kutokuridhika na usimamizi wa Serikali kwenye huduma za afya kunaweza pia kusababisha wananchi kutopendelea kwenda kupata matibabu na huduma katika vituo vya afya."*

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema kuwa "*Wazee na watoto wanaumia kwa sababu Sera hazitekelezwi. Mara nyingi sera zimebaki maneno matupu. Serikali inahitaji kutimiza ahadi zake za kufuatilia utekelezaji, kuwatunuku wanaotoa huduma nzuri, na kuwawajibisha wale wanaotoa huduma duni. Vinginevyo Serikali itapoteza uaminifu wake na watu maskini wataendelea kuteseka.*"

Mihutasari ya Twaweza inatoa matokeo mengine kadhaa na inaweza kupakuliwa kutoka [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)

---- Mwisho ----

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

Tunu Yongolo

Afisa Mawasiliano Twaweza

e: [tyongolo@twaweza.org](mailto:tyongolo@twaweza.org) | t: (+255) (0) 752 833 860

**Maelezo kwa Wahariri**

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo zinapatikana hapa [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org), au [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayomlenga raia na inayokusudia kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamaini kuwa mabadiliko ya kudumu hayana budi kuanzia chini kwenda juu. Tumedhamiria kujenga mazingira na kupanua fursa ambazo zitatoa mwanya kwa mamilioni ya watu kuhabarishwa and kuwawezesha kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao moja kwa moja na kuifanya serikali iwajibike.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:  
**Tovuti:** [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org) **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza\_NiSisi